

HALMASHAURI YA WILAYA YA UKERWE MKOA WA MWANZA

Phone + 255-0732-981174
Fax + 255-0732-981174
Email: ukerewedc@yahoo.com



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),
S.L.P 41,
NANSIO - UKERWE.

02.05.2017

TANGAZO LA ZABUNI Na. LGA 092/CTB/2016-17/11/13

KWA AJILI YA WATOA HUDUMA, WAPANGAJI KATIKA VYUMBA VYA BUCHA VYA HALMASHAURI VILIVYOPO SOKO KUU NANSIO, UPANGAJI KATIKA VYUMBA VYA BIASHARA VILIVYOPO STENDI KUU MPYA NANSIO (ambavyo havina wapangaji)

1. Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe inatangaza Zabuni tajwa hapo juu kwa watu binafsi, Vikundi, Kampuni au Mashirika yaliyo na vigezo vinavyostahili.

KUNDI A:-

- (a) Vifaa Tiba vya Hospitali.
- (b) Madawa ya binadamu.
- (c) Vifaa vya umeme/ umeme wa jua.
- (d) Pre-qualification Ujenzi wa Majengo / Matengenezo ya barabara.
- (e) Uchapishaji (Printing services).

KUNDI B:-

- (a) Upangaji katika vyumba vya Bucha Soko Kuu Nansio (kwa mwaka mmoja kuanzia **tarehe 01.07.2017 hadi tarehe 30.06.2018**).
- (b) Upangaji katika vyumba vya Migahawa Soko Kuu Nansio (kwa Mwaka mmoja kuanzia tarehe **01.07.2017 hadi tarehe 30.06.2018**).
- (c) Upangaji katika vyumba vya Biashara Stendi Kuu Nansio kwa muda wa mwaka mmoja kuanzia **tarehe 01.07.2017 hadi tarehe 30.06.2018**(Vyumba ambavyo havina wapangaji).

2. Njia itakayotumika ni ya Zabuni. Vitabu vya Zabuni vinapatikana Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) Idara ya Fedha kuanzia **saa 1:30 Asubuhi** hadi **saa 9:30 Alasiri** siku za kazi (Jumatatu - Ijumaa) isipokuwa siku za Sikukuu. Vitabu vitapatikana kuanzia tarehe **02.05.2017**.

3. Malipo kwa ajili ya Ununuzi wa Vitabu vya Zabuni yatakuwa kama ifuatavyo:-

• KUNDI A	(a - e)	Watalipa	Tshs. 100,000/=
• KUNDI B	(a na c)	Watalipa	Tshs. 100,000/=
• KUNDI B	(b)	Watalipa	Tshs. 30,000/=

4. Vitabu vya Zabuni halisi vilivyojazwa pamoja na nakala nyingine moja ziandikwe juu ya Bahasha Namba ya Zabuni. Pamoja na Jina la Zabuni inayoombwa mfano **"KUNDI A (a) Vifaa Tiba vya Hospital.**
5. Bahasha ziandikwe kwa **'Katibu wa Bodi ya Zabuni, Halmshauri ya Wilaya ya Ukerewe, S.L.P 41, Nansio - Ukerewe** na kisha zitumwe kwa Posta au zipelekwe kwenye Sanduku la Zabuni lililopo **Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, Ofisi ya Katibu Muhtasi wa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya** kabla ya saa 4:30 (saa nne na Nusu) asubuhi tarehe **24.05.2017** siku ya **Jumatano.**
6. Ufunguzi utafanyika tarehe **24.05.2017** baada ya saa **4:30** (saa nne na nusu) asubuhi katika ukumbi mkubwa wa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe. Waombaji au wawakilishi wao wanakaribishwa kwenye ufunguzi huu.
7. Waombaji wote wanatakiwa kuambatanisha vielelezo vyote muhimu vya biashara kwenye **vitabu vyao vya Zabuni, Leseni hai ya Biashara, TIN, Tax Clearance Certificate 20.06.2017, Bank statement ya mpaka tarehe 30.04.2017, Company Profile etc.**

NB. Kwa wakandarasi waonyeshe pia umiliki wa EFD Machine na Financial Audited Report 2015-2016.

8. Zabuni itakayochelewa, Zabuni za kielectronic, Zabuni ambayo haitapokelwa kwa muda na ambayo haitafunguliwa wala kusomwa wakati wa ufunguzi kwa vyovyote vile haitapelekwa katika ngazi ya Tathmini.

Wote mnakaribishwa,

MPURUGENZI MTENDAJI (W)

Bl. UKEREWE

.....
Frank S. Bahati
Mkurugenzi Mtendaji (W)
UKEREWE

Nakala kwa:-

- **Mamlaka ya Uthibiti wa Ununuzi wa Umma**
S.L.P 49,
Dar - es - Salaam.
- **Mkuu wa Wilaya,**
S.L.P 2,
Ukerewe.
- **Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe,**
S.L.P 41,
Nansio - Ukerewe